

KUMB: PPR/19 - 05/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 1 MEI 2019**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 1 Mei 2019**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Dar es Salaam**, zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Aprili 2019. Kwa mwezi Mei 2019, bei za rejareja za Petroli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 86/lita (sawa na asilimia 4.02) na Shilingi 13/lita (sawa na asilimia 0.63), mtawalia, wakati bei za Dizeli zimepungua kwa Shilingi 11/lita (sawa na asilimia 0.48). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 85.96/lita (sawa na asilimia 4.25) na Shilingi 13.08/lita (sawa na asilimia 0.66), mtawalia, wakati bei za Dizeli zimepungua kwa Shilingi 10.54/lita (sawa na asilimia 0.51). Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam yanatokana na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia kama inavyoonekana katika **Jedwali C** na kuongezeka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, sarafu ambayo hutumika kununulia mafuta.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Aprili 2019. Bei za Mafuta ya Taa hazijabadilika kwa sababu hakuna shehena ya bidhaa hiyo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga kwa mwezi wa Aprili 2019. Kwa mwezi Mei 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** zimeongezeka kwa Shilingi 149/lita (sawa na asilimia 6.97) na Shilingi 98/lita (sawa na asilimia 4.58), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 148.34/lita (sawa na asilimia 7.37) na Shilingi 97.79/lita (sawa na asilimia 4.85), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, ongezeko la bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga linatokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia na ongezeko la gharama za usafirishaji (*BPS premiums*) kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.
- (c) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Mtwara zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Aprili 2019. Kwa mwezi Mei 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini** zimeongezeka kwa Shilingi 171/lita (sawa na asilimia 8.05) na Shilingi 32/lita (sawa na asilimia 1.45), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 170.80/lita (sawa na asilimia 8.52) na Shilingi 32.19/lita (sawa na asilimia 1.53), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, ongezeko la bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Mtwara linatokana na mabadiliko ya bei za mafuta hayo katika soko la dunia, kama

inavyoonekana katika **Jedwali C**. Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

- (d) Ifahamike kuwa, tofauti za mabadiliko ya bei za mafuta kati ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara inatokana na tofauti za miezi ya kuingizwa mafuta nchini kupitia bandari hizo tatu kama inavyoonekana katika **Jedwali D**.
- (e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018**.**
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,233	2,181	2,109
Arusha	2,341	2,294	2,286

Arumeru (Usa West)	2,341	2,294	2,286
Karatu	2,359	2,312	2,304
Longido	2,352	2,305	2,297
Monduli	2,346	2,299	2,291
Monduli-Makuyuni	2,351	2,304	2,296
Ngorongoro (Loliondo)	2,425	2,379	2,371
Pwani (Kibaha)	2,238	2,186	2,114
Bagamoyo	2,244	2,192	2,121
Chalinze Junction	2,247	2,195	2,124
Chalinze (Msata)	2,252	2,199	2,128
Kibiti	2,254	2,202	2,130
Kisarawe	2,240	2,188	2,117
Mkuranga	2,243	2,191	2,119
Rufiji	2,261	2,209	2,137
Dodoma	2,292	2,240	2,168
Bahi	2,299	2,247	2,176
Chamwino	2,287	2,235	2,164
Chemba	2,318	2,266	2,195
Kondoa	2,325	2,273	2,201
Kongwa	2,289	2,237	2,166
Mpwapa	2,293	2,241	2,169
Mtera (Makatopora)	2,311	2,259	2,187
Geita	2,399	2,347	2,275
Bukombe	2,388	2,336	2,264
Chato	2,420	2,368	2,296
Mbogwe	2,437	2,385	2,313
Nyang'hwale	2,414	2,362	2,290
Iringa	2,297	2,245	2,174
Ismani	2,303	2,250	2,179
Kilolo	2,302	2,250	2,178
Mufindi (Mafinga)	2,307	2,255	2,184
Kagera (Bukoba)	2,449	2,397	2,325
Biharamulo	2,423	2,371	2,299
Karagwe (Kayanga)	2,465	2,413	2,341
Kyerwa (Ruberwa)	2,471	2,419	2,347
Muleba	2,449	2,397	2,325
Ngara	2,437	2,385	2,313
Misenyi	2,457	2,405	2,333
Katavi (Mpanda)	2,441	2,389	2,318
Mlele (Inyonga)	2,423	2,371	2,299
Mpimbwe (Majimoto)	2,433	2,381	2,310
Kigoma	2,465	2,413	2,341
Uvinza (Lugufu)	2,477	2,425	2,353
Buhigwe	2,454	2,402	2,330
Kakonko	2,422	2,370	2,298
Kasulu	2,451	2,399	2,327
Kibondo	2,429	2,377	2,305
Kilimanjaro (Moshi)	2,330	2,284	2,276

Hai (Bomang'ombe)	2,333	2,287	2,279
Mwanga	2,323	2,277	2,269
Rombo (Mkuu)	2,347	2,300	2,292
Same	2,317	2,270	2,262
Siha (Sanya Juu)	2,337	2,290	2,282
Lindi	2,312	2,268	2,168
Lindi-Mtama	2,317	2,273	2,186
Kilwa Masoko	2,336	2,292	2,143
Liwale	2,348	2,304	2,189
Nachingwea	2,332	2,288	2,198
Ruangwa	2,339	2,294	2,199
Manyara (Babati)	2,375	2,328	2,320
Hanang (Katesh)	2,385	2,339	2,331
Kiteto (Kibaya)	2,390	2,343	2,335
Mbulu	2,387	2,341	2,333
Simanjiro (Orkasumet)	2,407	2,360	2,352
Mara (Musoma)	2,412	2,360	2,288
Musoma Vijijini (Busekela)	2,453	2,401	2,329
Rorya (Ingirijuu)	2,421	2,369	2,297
Rorya (Shirati)	2,455	2,403	2,332
Bunda	2,403	2,351	2,279
Butiama	2,409	2,357	2,285
Serengeti (Mugumu)	2,457	2,405	2,334
Tarime	2,423	2,371	2,299
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,427	2,375	2,304
Mbeya	2,340	2,288	2,217
Chunya	2,350	2,298	2,226
Chunya (Makongolosi)	2,364	2,312	2,240
Kyela	2,356	2,304	2,232
Mbarali (Rujewa)	2,324	2,272	2,201
Rungwe (Tukuyu)	2,349	2,297	2,226
Morogoro	2,258	2,206	2,135
Mikumi	2,274	2,222	2,150
Kilombero (Ifakara)	2,296	2,244	2,172
Kilombero (Mlimba)	2,318	2,266	2,195
Kilombero (Mngeta)	2,308	2,256	2,184
Ulanga (Mahenge)	2,307	2,255	2,183
Malinyi	2,317	2,265	2,193
Kilosa	2,277	2,225	2,153
Gairo	2,277	2,225	2,153
Mvomero (Wami Sokoine)	2,269	2,217	2,145
Turiani	2,283	2,231	2,160
Mtwara	2,299	2,254	2,182
Nanyumbu (Mangaka)	2,335	2,291	2,231
Masasi	2,315	2,271	2,208
Newala	2,320	2,275	2,214
Tandahimba	2,313	2,268	2,207
Nanyamba	2,313	2,268	2,207

Mwanza	2,383	2,331	2,260
Kwimba	2,401	2,349	2,278
Magu	2,391	2,339	2,268
Misungwi	2,378	2,326	2,254
Sengerema	2,416	2,364	2,292
Ukerewe	2,443	2,391	2,319
Njombe	2,326	2,274	2,202
Njombe (Kidegembye)	2,346	2,294	2,223
Ludewa	2,364	2,312	2,240
Makambako	2,318	2,266	2,194
Makete	2,357	2,304	2,233
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,323	2,271	2,200
Rukwa (Sumbawanga)	2,406	2,354	2,282
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,406	2,354	2,282
Kalambo (Matai)	2,413	2,361	2,290
Nkasi (Namanyeke)	2,420	2,368	2,296
Ruvuma (Songea)	2,384	2,340	2,233
Mbinga	2,397	2,353	2,267
Namtumbo	2,375	2,331	2,262
Nyasa (Mbamba Bay)	2,422	2,378	2,277
Tunduru	2,350	2,305	2,292
Shinyanga	2,362	2,310	2,238
Kahama	2,376	2,324	2,252
Kishapu	2,391	2,339	2,267
Ushetu (Nyamilangano)	2,393	2,341	2,270
Simiyu (Bariadi)	2,404	2,352	2,280
Busega (Nyashimo)	2,397	2,345	2,273
Itilima (Lagangabilili)	2,407	2,355	2,283
Maswa	2,395	2,343	2,271
Meatu (Mwanhuzi)	2,402	2,350	2,278
Singida	2,324	2,272	2,200
Iramba	2,336	2,284	2,212
Manyoni	2,308	2,256	2,185
Ikungi	2,319	2,267	2,196
Mkalama (Nduguti)	2,348	2,296	2,225
Songwe (Vwawa)	2,350	2,298	2,226
Songwe (Mkwajuni)	2,356	2,304	2,233
Ileje	2,353	2,301	2,230
Momba (Chitete)	2,359	2,307	2,235
Tunduma	2,354	2,302	2,230
Tabora	2,387	2,335	2,264
Igunga	2,341	2,289	2,218
Kaliua	2,406	2,354	2,283
Ulyankulu	2,401	2,349	2,277
Nzega	2,352	2,300	2,228
Sikonge	2,399	2,347	2,276
Urambo	2,401	2,349	2,277
Uyui	2,388	2,336	2,265

Tanga	2,284	2,237	2,229
Handeni	2,305	2,258	2,250
Kilindi	2,320	2,273	2,265
Korogwe	2,296	2,250	2,241
Lushoto	2,305	2,259	2,251
Mkinga (Maramba)	2,291	2,244	2,236
Muheza	2,289	2,242	2,234
Pangani	2,291	2,244	2,236

JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,109.15	2,056.91	1,986.11

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,159.79	2,113.05	2,105.56

Bei za Jumla - MTWARA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,174.61	2,130.04	-----

JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

BANDARI YA DAR ES SALAAM

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 66.529/Tani	Ongezeko la Dola 18.283/Tani	Ongezeko la Dola 62.020/Tani
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Ongezeko la Dola 6.594/Tani	Punguzo la Dola 0.495/Tani	Ongezeko la Dola 0.920/Tani

BANDARI YA TANGA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 113.371/Tani	Ongezeko la Dola 73.638/Tani	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Ongezeko la Dola 12.160/Tani	Ongezeko la Dola 22.74/Tani	----

BANDARI YA MTWARA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 113.371/Tani	Ongezeko la Dola 62.338/Tani	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Ongezeko la Dola 5.380/Tani	Punguzo la Dola 8.080/Tani	----

**JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA
KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

	Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mafuta yalipokelewa mwezi wa:	DSM	Aprili 2019	Aprili 2019	Aprili 2019
	Tanga	Aprili 2019	Aprili 2019	Desemba 2018
	Mtwara	Aprili 2019	Aprili 2019	n/a
Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:	DSM	Machi 2019	Machi 2019	Februari 2019
	Tanga	Machi 2019	Machi 2019	Novemba 2019
	Mtwara	Machi 2019	Machi 2019	----
Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:	DSM	Februari 2019	Februari 2019	Januari 2019
	Tanga	Januari 2019	Januari 2019	----
	Mtwara	Januari 2019	Januari 2019	----

**Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA**